

Dawa za Kulevya ni Nini?

- Dawa za kulevya ni kemikali ambazo ziingiapo mwilini huathiri ubongo wa mtumiaji na kumsababishia kuwa na matendo, hisia, fikra na muonekano tofauti na matarajio ya jamii.
- Kemikali hizi hutokana na mimea na madini ambayo ni mali ghafi muhimu kwa mahitaji mengine ya mwanadamu. Dawa hizi huingia mwilini kwa njia kuu tatu:
 - o Njia ya kunywa / kula
 - o Kuvuta na
 - o Kujidunga sindano
- Dawa za kulevya ziko ambazo zimeruhusiwa kisheria kama tumbaku na pombe; ambazo hazijaruhusiwakamabangi, mirungi, cocaine, heroin na mandrax; na zinazoruhusiwa kwa matumizi ya hospitali kama Valium, pethedine, morphine n.k

Sababu Zinafanya Mtu Kutumia Dawa za Kulevya

Kuna sababu nyingi zinazoweza kumfanya mtu kutumia dawa za kulevya;

baadhi ni kama vile;

- o Kuiga tabia na kupenda kujaribu kutokana na ushawishi hasa wa kundi rika.
- o Kukosa shughuli ya kufanya
- o Magonjwa ya akili kama msongo wa mawazo
- o Kujiingiza kwenye starehe hasa klabu za usiku
- o Malezi mabaya ya kutoka kwa wazazi / walezi
- o Maradhi ya kimwili hasa ya muda mrefu
- o Mila na desturi mbali mbali
- o Msukumo wa maisha ya kisasa

Madhara ya kutumia Dawa za Kulevya

- Madhara ya kutumia dawa za kulevya aina ya dawa, kiasi cha dawa aliyotumika, uwepo wa ugonjwa wa akili, Umri wa kuanza kutumia, muda wa matumizi. Yapo madhara ya muda mfupi na muda mrefu.
- Madhara ya Muda Mfupi;
 - o Kuchangamka sana kuliko kawaida (cocaine na mirungi)

- o Kuzubaa, kulegea, kupepesuka au kulala (pombe, heroin)
- o Kuchanganyikiwa / kuehuka (bangi)
- o Kukosa usingizi, hamu ya kula na hamu ya kujamiana

• Madhara ya Muda Mrefu;

- o Kupoteza kumbu kumbu,
- o Kupoteza nguvu ya uzazi
- o Magonjwa ya akili, moyo, ini, mapafu, kiharusi, UKIMWI, magonjwa ya ngozi, utapiamlo nk.
- o Kuwa na tabia zisizokubalika kwenye jamii kama vile ukorofi, uongo, udokozi, wizi, chuki, lawama, visingizio, kukwepa majukumu na kukosa busara
- o Utegemezi wa dawa za kulevya

Utegemezi wa Dawa za Kulevya

- Utegemezi wa dawa za kulevya ni hali ambayo mtumiaji wa dawa hulazimika kutumia dawa kila siku ili kupata starehe na kujimudu. Utegemezi unaweza kuwa wa kisaikolojia au wa kimwili.

Utegemezi wa Kisaikolojia

- o Kuhangaika sana
- o Kuwa mwoga na mnyonge
- o Kutojiamani
- o Hasira na wasiwasi
- o Kushindwa kutekeleza wajibu
- o Mawazo hasi

Utegemezi wa Kimwili

- o Kukosa usingizi na hamu ya kula
- o Kutetemeka mwili
- o Kukosa hamu au kushindwa tendo la ndoa
- o Kutokwa jasho
- o Kuharisha
- o Kushindwa kuongea vizuri
- o Kuumwa kichwa
- o Kupiga miayo mara kwa mara

Kitu Gani Kifanyike kwa Watumiaji wa Dawa za Kulevya?

- Elimu ni kitu cha msingi, watu waelimishwe kuanzia utoto wao ili katika maisha yao wafanye uchaguzi sahihi wakifahamu.
- Tiba sahihi na ya mapema
 - o Tiba ya kisaikolojia (kujitambua aliko, anapotaka kuwa na kuamua kufanya mabadiliko kwa kutegemea uwezo wake

mwenyewe

- o Tiba kimwili kutumia dawa za hospitali
- o Matibabu kwenye nyumba za upataji nafuu (Sober Houses)
- Ushirikiano kati ya mgonjwa jamii au ndugu na wataalam ni muhimu sana katika matibabu ya watu wanaotumia dawa za kulevya.

Piga vita matumizi ya dawa za kulevya kwani zinaharibu nguvu kazi ya familia na Taifa kwa ujumla.

Kwa taarifa za zaidi wasiliana na
Kituo cha Afya
Simu namba 2410014
Barua pepe: healthcentre@udsm.ac.tz



CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

KITUO CHA AFYA

S. L. P 35074 DAR ES SALAAM



MADHARA YA DAWA ZA KULEVYA